13. Ikiwa tutakataa kutembea katika nuru, ni nini tutaweza kutarajia? Waefeso. 5: 6; 2 Wathes. 2: 10-12.
14. Ikiwa tunasema kwamba sisi ni WaMasihi na tunaenenda katika giza ni nini tunayoonyesha? 1 Yohana 1: 6.
15. Tutaenenda kwa jinsi gani kwa ndugu ikiwa tutatembea katika nuru? 1 Yohana 2: 9-11.

******************************

**Somo la Machi 15, 2025 (Adar 15, 5785)**

## KUITWA KWA KAZI MAALUM KWA WAKATI MAALUM

**Somo Kuu: Ufunuo sura ya 16.**
**Fungu La Kukariri: Ufunuo 16: 1.**

1. Ni juu ya nani ambaye pigo la kwanza kati ya yale mapigo saba ya mwisho lilimwagiwa? Ufunuo 14:9, 18: 4.
2. Ni ishara gani mbili zimepeanwa kwa wakati huu maalum wa maandalizi? Nahumu 2:3.
3. Kumekuwa na jumbe tatu kwa dunia yote, ambazo zilitumwa tangu mwanzo wa injili. Ni nini na ni wakati upi ujumbe wa kwanza ulitolewa? Ufunuo 14: 6.

   **Maelezo**: Huu ulikuwa ujumbe uliotumwa mbele katika siku za Mitume, katika ulimwengu



**Somo La Januari 25, 2025 (Tevet 25, 5785)**

## WAFANYA KAZI PAMOJA NA MASIHI YAHSHUA

**Somo Kuu: Mathayo 25: 14-30.**
**Fungu La Kukariri: Mathayo 25:30.**

1. Je! Ni kwa sababu gani sisi sote tumeumbwa na kufanywa viumbe vipya? Waefeso 2:10.
2. Je! Ni swali gani Bwana huwauliza wale ambao hawajishughulishi na kazi yake? Mathayo 20: 6.
3. Je! Yeye anawaamuru wafanye nini? Mathayo 20: 7.
4. Je! Watafanywa nini wale wanaokataa kumheshimu Elohim kwa kuzaa matunda katika shamba lake la mizabibu? Yohana 15: 2.
5. Ni kwa njia gani Bwana anawahimiza wale ambao hawaoni kazi ya kufanywa? Yohana 4:35, 36.
6. Je! Bwana alisema nini kuhusu mavuno na wafanya kazi? Mathayo 9:37.
7. Je! Bwana anasema nini kwa wale ambao tayari wanashiriki katika kazi ya Bwana? Mathayo 9:38.
8. Je! Ni kiasi gani kinachookolewa ikiwa kazi yetu inasababisha kugeuzwa kwa mwenye dhambi mmoja kutoka kwa makosa ya njia yake? Yakobo 5:20.





***"Utakieni Yerusalemu amani; Na wafanikiwe wakupendao" Zaburi 122:6***



# Masomo Ya Bibilia

***kwa***

**KANISA LA ELOHIM (COG)**
**Siku Ya Saba (7th day)**

Robo Ya Kwanza
2025

Ya
Januari, Februari, Machi.
**(Tevet, Shevat, Adar)**

Watenda kazi wanahitajika,
Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache...

**Tuma maombi yote kwa S.L.P 568, Jerusalem — Israel**

9. Nafsi moja ina thamani gani? 1 Wakorintho 3: 9,10.
10. Je! Wokovu wa roho moja unatosha kuwafanya malaika wa mbinguni wafurahi? Luka 15:10.
11. Je! Paulo anasema nini juu ya mfanyakazi? 1 Wakorintho 3: 9,10.
12. Je! Ni uhakikisho gani unaopewa wale wote ambao ni wafanyakazi wenza na Bwana? 1 Wakorintho 15:58.
13. Je! Tunapaswa kuomba nini ili kufanikiwa katika kazi hii Kubwa? Zaburi 51: 9-13.
14. Je! Ni nani tunapaswa kujifunza naye jinsi ya kufanya kazi iliyo na mafanikio? Mathayo 11: 29, 30.

*******************************

**Somo La Februari 1, 2025 (Shevat 3, 5785)**

## WAFANYA KAZI WENYE MANUFAA PAMOJA NA MASIHI YAHSHUA

**Somo Kuu: Yohana 15: 1-5.**
**Fungu La Kukariri: Yohana 15:5.**

1. Je! Yahshua aliwaitaje wale aliowaita kufanya kazi katika shamba lake la mizabibu? Mathayo 4:19.
2. Je! Mitume walifanikiwa sana bila Mwokozi? Yohana 21: 3-5.



4. Je, Yahshua alisema watu wake ni nini? Kwa nini watu huweka taa katika maeneo ya giza? Mathayo. 5:14-16.
5. WaMasihi watatumiaje mwanga ambao Elohim amewapa? 2 Wakor 4:6; 1 Peter. 2:12.
6. Je! Ni hatari gani inayotishia wale wasiotembea katika nuru? Yohana 12:35.
7. Watu wa Elohim wanaionaje Biblia, Neno Takatifu la Elohim? Zab. 119: 105; 12: 6.
8. Ni kundi gani la watu hujikwaa? Lini? Yohana 11: 9, 10; Mathayo. 15:14.
9. Je, Yahshua na Neno huweza kutenganishwa? Yohana 1: 4, 14.

**Maelezo**. - Tunaona kwamba mwanzoni Yahshua alikuwa Neno, na Neno ni taa na nuru kwa wote ambao Bwana amewachagua. Kwa hivyo, tunapaswa kutarajia kwamba watu wa Bwana wataendelea kuamini na kulithamini Neno, na si kwa kugawanya neno kama tunavyopata wengi wanafanya wakati huu wa sasa.

10. Yahshua alisema nini kuhusu mwanga? Yohana 8:12.
11. Je! Watu waliozaliwa tena wanaruhusiwa kutembea gizani au kuwa na ushirika na wale hutembea katika giza? Waefeso. 5:11; Warumi. 13:12; 2 Wakor. 6:14.
12. Je, ni ushauri gani Paulo aliwapa ndugu wa Filipi? Wafilipi. 2:15.



**Somo La Januari 4, 2025 (Tevet 4, 5785)**

## KAZI ILIYO NA UTUKUFU NA THAWABU

**Somo Kuu: 1 Wakorintho 15:41-58.**
**Fungu La Kukariri: 1 Wakorintho 15:28.**

1. Je! Tunapaswa kuvumilia nini tukiwa askari wa Masihi Yahshua? Luka 21:16,17.
2. Je! Watenda kazi wa Bwana wanapaswa kuvikwa nini? Waefeso 6:10-18.
3. Je! Shamba la Bwana ni lipi (ambalo kila mshirika wa kanisa ni mtenda kazi)? Mathayo 13:38.
4. Je! Tunapaswa kutumia nini katika kazi ya Bwana? Marko 4:14.
5. Ni wapi katika shamba hili kuu? Tutafanya wapi kazi hii yote muhimu? Mhubiri 11:1, 2; Luka 14:21, 23 .
6. Ni mfano gani wa kufanya kazi ambao umetolewa kwetu kama ulivyoonyeshwa na Bwana na mitume kuhusu kufanya kazi nyumba kwa nyumba? Luka 5:29-32; 7:36; 19:1-5; Matendo 20:20.
7. Je! Tutafanya kazi lini? Mhubiri 11:6.
8. Je, wale wanaofanya kazi katika hali ya hewa nzuri tu wana ahadi ya mavuno mazuri? Mhubiri 11:4.



hamu ya kutosha katika kweli kujifunza wenyewe.

12. Yahshua alituonyaje kuhusu wadanganyi katika siku hizi za mwisho? Mathayo. 24: 4, 5, 11, 24.
13. Ni jinsi gani tutazijaribu roho? Isa. 8:20.
14. Ni katika msingi gani tunapaswa kujenga ili tuwe na uhakika kwamba hatutaweza kudanganywa? Waefe. 2:20, 21.
15. Makuhani wengine (Wahudumu) wataonyeshaje kutokubali ukweli wa Neno Takatifu la Elohim? Eze. 22:26.

******************************

hii, itakuwa na matokeo kwa jinsi ya kimwili ilivyo badala ya ukuaji kwa njia ya kiroho. Mambo ya Elohim yanaeleweka kwa njia kiroho: kwa hivyo, tuliona karama za Roho Mtakatifu zinahitajika ili kuelewa vizuri na kupokea tafsiri sahihi ya maandiko.

6. Je, karama ya nne ya Roho Mtakatifu ni ipi? Mstari wa 9, sehemu ya mwisho.
7. Je, karama zingine za Roho Mtakatifu ni zipi? Mstari wa 10.
8. Je! Kila mtu anayeunganishwa na mwili wa Masihi ana baadhi ya karama za Roho Mtakatifu? Mstari wa 11, sehemu ya mwisho.

*******************************

**Somo la Machi 8, 2025 (Adar 8, 5785)**

## KUNG'AA KWA AJILI YA YAHSHUA

**Somo Kuu: 1 Thes. 5.**
**Fungu La Kukariri: Yohana 8:12.**

1. Ni nani ambaye ni mwanga wa ulimwengu? Je! Wale hutembea watafuataje nuru? Yohana 8:12, 9: 5.
2. Yahshua alifanyaje mwanga wake kuangaza? Matendo 10:38.
3. Ni nini kilichosemwa kuhusu miji aliyotembelea? Mathayo. 4:16.



3. Je! Yahshua aliwaambia wanafunzi wake wafanye nini? Je! Walifanikiwa? Yohana 21: 6.
4. Je! Inawezekana kwa wajumbe kupata mafanikio yoyote bila msaada wa Bwana Yahshua Masihi? Yohana 15: 5.
5. Je, MMasihi yeyote anaweza kuwa mfanyakazi katika shamba la mizabibu la Bwana? Luka 9:49, 50.
6. Mtumishi wa Bwana anapaswa kuwa katika hali gani? 2 Timotheo 2: 22-25.
7. Je! Paulo alisema aliogopa angepata nini kati ya ndugu wa Korintho? 2 Wakorintho 12:20.
8. Je! Maagizo ya Yakobo kwa WaMasihi ni gani? Yakobo 2:17, 18.
9. Paulo alitoa maagizo gani? Na ni mfano gani tunapaswa kuonyesha? 1Timotheo 4: 12-16.
10. Je! Petro alisema tunapaswa kufanya nini? 1 Petro 3:15.
11. Jinsi gani tutaweza kumtukuza Baba yetu wa Mbinguni? Yohana 15: 8.
12. Je! Bwana anasema nini kwa wale ambao hawaoni kazi ya kufanywa? Yohana 4:35, 36.

*******************************



3. Je! Wanafunzi walielewa injili au ujumbe wa Masihi kwa mara ya kwanza? Luka 9: 51-56.
4. Hata baada ya Pentekoste, Petro alishindwaje kuliongoza Kanisa? Wagal. 2: 11-13.
5. Ni kwa njia gani watu hudanganywa kwa urahisi? 2 Petro 2: 1-3.
6. Je, ni hali gani mbaya ambayo ilifanyika Korintho ambayo inaweza kuwa matokeo ya udanganyifu? 1 Wakor. 1: 11-13.
7. Ni nini baadhi ya watu ambao waliokuwa wameamini walijaribu kuleta kwa kanisa wakati wa Paulo? Wagal. 4: 8-11; Matendo 15: 5.
8. Ni kwa maneno gani yenye nguvu ambayo Paulo alitumia kupinga mafundisho haya? Matendo 15:10.
9. Je, ni hali gani ya wakati wa leo ilizuia hata kanisa la kwanza? 3 Yohana 9, 10.
10. Yohana aliwaonyaje WaMasihi kuhusu manabii wa uongo katika siku zake? 2 Yohana 6, 7.
11. MMasihi anapaswa kufanya nini ili kujua ukweli na kutopotoshwa? 1 Yohana 4: 1

**Maelezo**. Wale ambao hudanganywa kwa hiari yao wanaweza kugawanywa katika makundi mawili; wale wanaopenda mapokeo ya wanadamu vizuri sana hivi kwamba wanakataa kuzingatia ushahidi kutoka kwa Biblia, neno takatifu la Elohim, ambalo linaweza kuvuruga mawazo yao ya sasa, na wale ambao hawana



9. Ni kwa nini tunapaswa kushiriki katika kazi hii kubwa bila kukawia? Yohana 9:4.
10. Je, kila moyo unapaswa kujaa huruma na upendo kwa wale ambao wanafanya kazi kwa ajili yao? Zaburi 126:5,6.
11. Ni ahadi gani kubwa inayotolewa kwa wale wanaogeuza watu kwa utakatifu? Danieli 12:3.
12. Sisi tukiwa wanafunzi wa Masihi tutaweza kuthibitishaje kwamba sisi ni wanafunzi? Yohana 15:8.
13. Ni kweli gani mbili za ajabu tunapaswa kuelewa tunapofanya kazi katika shamba Lake la mizabibu? Isaya 55:10-11; 1 Wakorintho 13:8.

*******************************

**Somo La Januari 11, 2025 (Tevet 11, 5785)**

## MSIMAMIZI MWAMINIFU

**Somo Kuu: Luka 16: 1-15**
**Fungu La Kukariri: Luka 16:10**

1. Ni mbinu gani Yahshua alitumia sana katika mafundisho yake? Marko 4:33, 34.
2. Katika mfano wa msimamizi, alishitakiwa na nini? Luka 16: 1.
3. Msimamizi aliulizwa afanye nini? Luka 16: 2.
4. Wasimamizi wanafaa kuhitaji nini? 1 Wakor. 4: 2.

**Somo La Februari 8, 2025 (Shevat 10, 5785)**

## KUPELEKA MWANGA WA KWELI

**Somo Kuu Mat: 25: 1-30**
**Fungu La Kukariri: 1 WaKor. 15:58**

1. Yahshua aliwaita watu fulani wafanye kazi gani? Mat. 4:17-22
2. Alisema nini kuhusu mavuno na watenda kazi? Mat. 9:36-38.
3. Mwisho utakuja lini? Mathayo 24:14
4. Je! Ni amri gani maalum aliyotupa? Math 28:18-20
5. Jinsi gani kazi ya Bwana ni ya dharura? Luka 14:23
6. Je! Mtu anapaswa kufanya nini ili awe mfanyakazi wa Masihi Yahshua? Math 16:24
7. Ni ahadi gani inayotolewa kwa wafanyikazi wenye bidii? Zaburi 126: 5, 6
8. Jinsi gani ni muhimu kujibu wito wa injili? Eze. 33: 7-19
9. Je! Tunaweza kufanya uchaguzi wetu ikiwa tutahubiri injili au la? 1 WaKor. 9:16
10. Ni mpangilio gani ambao Elohim alifanya ili wote washiriki katika kuleta injili kwa wenye dhambi? Mat. 14:30

**Maelezo**. Elohim huwaita watu fulani watumie wakati wao wote katika shamba lake la



1. Je! Ni mapenzi ya Elohim kwamba kanisa lake liweze kujua kuhusu karama maalum za Roho Mtakatifu? 1 Wakorintho 12: 1.
2. Ni nini kilichosemwa kuhusu tofauti za karama, na udhihirisho wa Roho Mtakatifu? Mstari wa 6, 7.
3. Ni nini kilichosemwa kuhusu aina tofauti za utendaji na uongozi wa Roho Mtakatifu? Mstari wa 4, 5.

**Maelezo** . Udhihirisho wa Roho Mtakatifu hutolewa bila shaka kwa faida, na ukweli kwamba Elohim hawezi kubadilika kwa namna yake au jinsi hushughulika kwa mtu binafsi huthibitisha kwamba nguvu hiyo hiyo, ambayo ilionekana wakati huo katika aina hizi za karama, bado inaonekana kati ya wana wa Elohim.

4. Ni karama gani za kwanza za Roho Mtakatifu ili mtu azipate? Mstari wa 8.
5. Je, karama ya tatu ya Roho Mtakatifu ni ipi kwa utaratibu wake wa mahitaji maalum, ambayo hekima na maarifa ya Neno hutusaidia kupata? Sehemu ya kwanza ya mstari wa 9; Warumi. 10:17

**Maelezo.** Itasisitizwa kwamba imani ni moja ya karama maalum ya Roho ambayo huja kama matokeo ya karama mbili zizotangulia za hekima na maarifa. Bwana anatoa maagizo pia ya kujifunza (2 Tim 2:15), lakini isipokuwa Roho Mtakatifu atafutwe na kupatikana kwa ajili ya kazi



**Maelezo**. Msimamizi ni mtu anayeweza kusimamia au anayesimamia bidhaa za mtu mwingine. Kama vile viongozi wa kidunia wanapaswa kuwajibika kwa mabwana wao, pia nasi kwa Elohim. Siku moja tutahitajika kuwajibika katika uongozi wetu kwake.

5. Ni sehemu gani ya mapato yetu ambayo Bwana anahitaji? Walawi. 27:30, 32.
6. Ni kiasi gani cha zaka kinachopaswa kuletwa kwenye hazina ya Bwana? Malaki 3:10.
7. Tunawezaje kumwibia Elohim? Je, matokeo yake ni nini? Mai. 3: 8, 9.

**Maelezo**. Ikiwa tumeajiriwa kwa kibarua au mshahara, tunafanya kazi katika kilimo au sekta nyingine yoyote, sisi ni wasimamizi tu juu ya mapato yetu.

8. Je! Elohim aliahidi ulinzi maalum kwa wakulima ambao ni waaminifu katika kutoa fungu la kumi? Mal. 3:11.
9. Tunaposhindwa kulipa zaka, nini kinachotokea kwa wahudumu? Neh. 13:10.
10. Iwapo kanisa litakosa kutoa fungu la kumi, viongozi wanapaswa kufanya nini? Neh. 13:11.
11. Mtume Paulo anasema nini kuhusu watumishi wanaopokea zaka? 1 Wakor. 9: 9-11, 13.
12. Paulo aliomba msamaha kwa ndugu wa Korintho; Ni kwa nini? 2 Wakor. 11: 7, 8 na 12:13.



6. Ni kwa mara ngapi mtu wetu wa kiroho anafaa kufanywa awe mpya? 2 Wakorintho 4:16.
7. Ni somo gani tunapaswa kujifunza kwanza? Isaya 40:31.
8. Ni katika mfano wa nani tunapaswa kufanywa upya? Kol. 3:10.
9. Katika kufuata Masihi tunapaswa kutafuta kutenda mapenzi ya nani? Yohana 5:30.
10. Ni jaribio gani la MMasihi linaloonekana kwa wote? 1 Yohana 2: 15-17.
11. Tito 3: 5 ni kweli, ni nini tunapaswa kuwa makini kwayo? 1 Yohana 2:28.
12. Ili kuishi maisha ya kushinda ni hatua gani zinahitajika? Wafilipi 1: 9-11.

*******************************

**Somo la Machi 29, 2025 (Adar 29, 5785)**

## MAFUNDISHO YA UONGO NYAKATI ZA MWISHO

**Somo Kuu: 1 Wakor. Sura ya 3.**
**Fungu La Kukariri: Warumi. 16:17.**

1. Je, kuna hatari ya kudanganywa? Wakolosai. 2: 8; 1 Yohana 4: 1
2. Je, kutatendeka nini kwa wale wanaofuata mafundisho ya mwanadamu? Wakolosai. 2: 20-22.

7. Je! Ni nini kilichosemwa kuhusu kiasi cha uponyaji kilichofanywa jioni ilipofika? Mathayo 8:16.
8. Hilo lilitimiza unabii gani? Mathayo 8:17; Isaya 53:3-6.
9. Uponyaji huo ulitimizwa kupitia nguvu gani? Isaya 61:1; Matendo 10:38.
10. Ni tukio gani lingine lililofuata? Je, wanafunzi walikuwa na mawazo gani kuhusu nini kingekuwa sehemu yao? Je, walimwomba Yahshua nini? Jadili Mathayo 8:22-27.
11. Yahshua alikutana na nani baadaye? Mathayo 8:28.
12. Je, pepo walimjua Masihi? Mathayo 8:29.
13. Je! Ni nini kilifanyika baadaye? Mathayo 8:31,32.
14. Watu wa jiji walilichukuliaje jambo hilo? Mathayo 8:33, 34.

*******************************

**Somo la Machi 1, 2025 (Adar 1, 5785)**

## UMUHIMU WA KARAMA ZA ROHO MTAKATIFU

**Somo Kuu: 1 Wakor. 12**
**Fungu La Kukariri: Mika 3: 8**



mizabibu, lakini sio wote wanaweza kuhubiri; bado ana kitu cha kufanya kwa kila mshirika wa mwili, ili kuwa mtumishi mwenye faida. Mtume Paulo aliwaambia ndugu wa Korintho (dada wakiwemo) kuwa wazidi katika kazi ya Bwana - 1 WaKor. 15:58

11. Je! Kila mmoja anaweza kushiriki vipi katika kueneza injili hata kama yeye mwenyewe hawezi kwenda? 2 Wakor 9: 1-7
12. Je! Imewekwaje kwa watenda dhambi kusikiliza injili? Warumi 10: 14,15
13. Je, mhudumu anatarajiwa kwenda kwa malipo yake mwenyewe, au atarajie msaada wakati anafanya kazi katika shamba la mizabibu la Bwana. 1 WaKor 9: 7-11; Warumi 15:27
14. Je! Elohim alitoa mpango gani ili wahudumu wake watimiziwe mahitaji yao? 1WaKor. 9: 13-14, Hes. 18:21
15. Wakati Paulo alipowavuta wenye dhambi kwake Masihi, je! Aliuchukua utukufu mwenyewe au alitukuza wale waliomsaidia? Phil. 4: 14-17.

*******************************



**Somo la Machi 22, 2025 (Adar 22, 5785)**

## MAISHA YA USHINDI

**Maelezo**: Wengi wanasema kuwa ukamilifu ni kiwango cha juu sana kufikia, kwamba haiwezekani kufikia. Kuna, hata hivyo, mifano mingi katika Biblia ya watu ambao waliishi kulingana na mapenzi ya Elohim. Katika Masihi Yahshua yote yanawezekana. "Naweza kufanya mambo yote kupitia Masihi ambaye hunitia nguvu," ilikuwa ushahidi wa mtu ambaye alienenda na Elohim. Wafilipi 4:13. Maisha ya ushindi huja kama matokeo ya upinzani wa mara kwa mara kwa majaribu ya shetani. Masihi alikumbana na majaribu yote kwa jibu la Maandiko katika kumkataa Shetani jangwani. Kufuatia mfano wake tunapaswa kuongozwa na viwango vya Biblia tunapopigana dhidi ya uovu wa kiroho mahali pa palipoinuka.

**Somo Kuu: Wafilipi 1: 1-20.**
**Fungu La Kukariri: Warumi 6: 1-4.**

1. Je! Ni nini inatarajiwa kwetu katika dunia hii mbaya? Tito 2: 11,12
2. Je! Hii inawezekanaje? 1 Yohana 5: 5-7.
3. Je! Ni watu gani wanaoishi kama mfano mzuri wa maisha ya ushindi? Waebrania 11: 5; Luka 1: 5,6.
4. Je! Ni hatua gani muhimu inahitajika katika mioyo yetu? 1 Petro 3:15.
5. Tunapompinga Ibilisi, ni nini tumehakikishiwa? Yakobo 4: 7,8.



**Maelezo**. Ikiwa sisi ni wasimamizi waaminifu, hakika Elohim atatubariki. Zaburi 50:14, 15.

*******************************

**Somo La Januari 18, 2025 (Tevet 18, 5785)**

## MAFUNDISHO YA UTUMISHI UAMINIFU

**Somo Kuu: Tito 1: 1-15.**
**Fungu La Kukariri: Tito 2: 1.**

1. Je! Mtume Yuda alisema ni nini tunapaswa kushindania kwa bidii? Yuda 3.
2. Je! Kuna aina gani mbili za mafundisho ulimwenguni? Mat. 7:28, 29; 1 Tim. 4: 1.

   **Maelezo**. Katika maandiko haya mawili yametajwa mafundiko ya Masihi, na mafundisho ya mashetani.

3. Je! Mafundisho ya Masihi ni gani kulingana na 1 Tim 6: 3-5?
4. Je Yahshua alisema nini juu ya mafundisho yake? Yohana 7:16.
5. Kwa nini alisema hivi? Yohana 6:38; 5:30.
6. Jinsi gani na ni kupitia njia gani tutaweza kujua mafundisho ya kweli? 2 Tim. 3:16, 17.
7. Je! Roho Mtakatifu hufanya kazi kupitia njia gani kufunua ukweli wa ajabu wa kuokoa? 2 Pet. 1:20, 21; Waebrania 10:25; Ufu. 2: 7.

**Somo la Februari 15, 2025 (Shevat 17, 5785)**

## MATUNDA KWENYE MSIMU UNAOFAA

**Somo Kuu: Mathayo 25:14-30.**
**Fungu La Kukariri: Mathayo 25:30.**

1. Je, Elohim anatarajia kupokea matunda kutoka kwa watenda kazi wake? Mathayo 21:34; Mathayo 25:20-23.
2. Je! Tutafuata na kutamani nini? 1 Wakorintho 14:1.
3. Tunaposikia Neno na kulielewa, tunapaswa kufanya nini? Mathayo 13:23.
4. Atafanya nini kwa baadhi ya wasiozaa matunda? Mathayo 21:41; 25:28-30.
5. Je, tunaonywaje kuhusu wokovu wa kustarehesha? Luka 3:8,9.
6. Je, kuna hekima ambayo pia itazaa matunda? Yakobo 3:17.
7. Ni ipi mojawapo ya njia za kutambua mafundisho ya uwongo? Mathayo 7:16-20.
8. Jinsi gani tutaweza kupokea karama za Roho Mtakatifu? Luka 11:13.
9. Je! ni kwa sababu gani tunapaswa kutafuta Karama za Roho? 1 Wakorintho 14:12. Soma pia Wakolosai 1:9,10.
10. Ni aina gani ya matunda tunapaswa kuzaa ikiwa tunataka kuwa na Roho wa Elohim? Wagalatia 5:22,23. Soma pia Waefeso 5:9.



**Maelezo**. Pamoja na kila kazi kuna mahitaji ya kuzalisha kiasi fulani cha matunda. Tunapokubali Ufalme wa Elohim tunakubali pia jukumu la kutumikia chini ya uongozi wa Masihi. Kupitia Roho wa Elohim tunatumwa kama watenda kazi katika shamba lake la mizabibu. Kwa hiyo, ni muhimu kumtolea matunda kwa wakati wake. Tutumie vipaji vyetu vyema na tusisahau wito tulioitiwa.

******************************

**Somo la Februari 22, 2025 (Shevat 24, 5785)**

## UPONYAJI: KUTOA PEPO

**Somo Kuu: Mathayo 8.**
**Fungu La Kukariri: Mathayo 8:17.**

1. Je! Ni nani aliyekuwa wa kwanza kuponywa baada ya mahubiri ya Masihi mlimani? Mathayo 8:1-3.
2. Je! Ni nani baadaye aliyeomba uponyaji kwa Masihi Yahshua? Mathayo 8:5,6.
3. Je! Ni imani gani isiyo ya kawaida aliyoonyesha? Mathayo 8:7-9.
4. Mwokozi alilichukuliaje jambo hili? Je, alitoa maoni gani? Mathayo 8:10-12.
5. Imani yake ilituzwaje? Mathayo 8:13.
6. Mama-mkwe wa Petro aliponywa kutokana na nini, na kwa njia gani? Mathayo 8:14,15.



8. Je! Utii wa mafundisho ya kweli utatusaidia? Warumi 6:17, 18.
9. Kama watoto wa Elohim na waalimu, tumeagizwa kufundisha nini? Tito 2: 1.
10. Je! Mafundisho ya kweli yanapaswa kulaani aina zote za dhambi? Dhambi ni nini? 1 Tim. 1: 9-10.
11. Je! Kwa mafundisho ya kweli tutaweza kufanya nini? Tito 1: 9.
12. Ikiwa tutazingatia mafundisho ya kweli ya Biblia, yatafanya nini? 1 Tim 4:16.
13. Masihi Yahshua alituamuru nini tusiache kufanya nini? Mat. 23:23.
14. Ni kwa nini watu walishangazwa na mafundisho ya Masihi? Mat. 7:28, 29.

    **Maelezo**. Masihi alinena kwa mamlaka kwa sababu alifundisha Neno katika usafi wake, na hakuna mpinzani aliyetegemea mafundisho ya uwongo aliyeweza kuyapinga hayo; ndivyo ilivyo kwa kila mtu leo ambaye anaweza kuchukua Neno ambalo halijachafuliwa kama mwongozo wake.
15. Je! Ni kwa vipi Paulo alisema wengine watazingatia mafundisho ya kweli katika siku zijazo? 1 Tim. 4: 1-4.

******************************



wa waabuduo sanamu ili kuharibu sanamu zao na kumwabudu yeye aliyeziumba mbingu na dunia. Ilikuwa pia saa ya hukumu juu ya taifa la Wayahudi (Luka 21:24), na juu ya mkuu wa ulimwengu huu.

4. Ni nini imesemwa kuhusu wakati wa hukumu ambayo ilikuwa sehemu ya ujumbe wa kwanza kwa dunia yote? 1 Petro 4:17; Yohana 16:7-11; 12:31.
5. Je! Asili ya ujumbe wa malaika wa pili ni nini? Ufunuo 14: 8.
6. Je! Asili ya ujumbe wa malaika wa tatu ni nini, na ni juu ya nani hasa umeelekezwa? Ufunuo14:9, 10.
7. Je, ni tukio gani linalofuata ujumbe huu? Kuna ujumbe mwingine bado utapeanwa, au ni wakati wa mfalme kuja na kutawala? Ufunuo 14:14-16.
8. Je, Ufunuo 15:1 pia inatuambia nini kuhusu mapigo haya ya mwisho?

**Maelezo**: Ujumbe wa kumtambua mnyama, na kutoa tahadhari hii, ni “chakula cha wakati unaofaa”. Ni ujumbe huu ambao umefika wakati wake katika ulimwengu kwa wakati huu maalum.

******************************